

**KUMB: PPR/18 - 11/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 NOVEMBA 2018**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 7 Novemba 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Oktoba 2018. Kwa mwezi Novemba 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 29/lita (sawa na asilimia 1.22), Shilingi 81/lita (sawa na asilimia 3.52) na Shilingi 34/lita (sawa na asilimia 1.50), mtawalia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 28.74/lita (sawa na asilimia 1.28), Shilingi 80.90/lita (sawa na asilimia 3.71) na Shilingi 33.58/lita (sawa na asilimia 1.58), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premium*).
- (b) Vilevile, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Oktoba 2018. Bei za Mafuta ya Taa katika ghalaa la mafuta mkoani Tanga hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena mpya ya Mafuta ya Taa iliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Oktoba 2018. Katika toleo hili, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 87/lita (sawa na asilimia 3.72) na Shilingi 111/lita (sawa na asilimia 4.89), mtawalia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 87.18/lita (sawa na asilimia 3.92) na Shilingi 110.58/lita (sawa na asilimia 5.15), mtawalia. Ongezeko hili la bei za mafuta katika ghalaa la mkoani Tanga limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta (*BPS Premiums*).
- (c) Hakuna shehena mpya ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Mtwara katika mwezi wa Oktoba 2018. Hivyo, katika mwezi wa Novemba 2018, bei za Petroli na Dizeli mkoani Mtwara, Lindi na Ruvuma zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Oktoba 2018. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.
- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuvi ya bidhaa za mafuta.
- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017**.**
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuvi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuvi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

#### A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,396</b>	<b>2,385</b>	<b>2,280</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,492</b>	<b>2,437</b>	<b>2,282</b>
Arumeru (Usa West)	2,492	2,437	2,282
Karatu	2,510	2,456	2,300
Longido	2,503	2,448	2,293
Monduli	2,497	2,443	2,287
Monduli-Makuyuni	2,502	2,447	2,292
Ngorongoro (Loliondo)	2,577	2,522	2,366
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>2,401</b>	<b>2,390</b>	<b>2,285</b>
Bagamoyo	2,408	2,396	2,292
Chalinze Junction	2,411	2,399	2,295
Chalinze (Msata)	2,415	2,404	2,299
Kibiti	2,417	2,406	2,301
Kisarawe	2,404	2,392	2,288
Mkuranga	2,406	2,395	2,290
Rufiji	2,424	2,413	2,308
<b>Dodoma</b>	<b>2,455</b>	<b>2,444</b>	<b>2,339</b>
Bahi	2,463	2,451	2,347

Chamwino	2,451	2,439	2,335
Chemba	2,482	2,471	2,366
Kondoa	2,488	2,477	2,372
Kongwa	2,453	2,441	2,337
Mpwapwa	2,456	2,445	2,340
Mtera (Makatopora)	2,474	2,463	2,358
<b>Geita</b>	<b>2,562</b>	<b>2,551</b>	<b>2,446</b>
Bukombe	2,551	2,540	2,435
Chato	2,583	2,572	2,467
Mbogwe	2,600	2,589	2,484
Nyang'hwale	2,577	2,566	2,461
<b>Iringa</b>	<b>2,461</b>	<b>2,449</b>	<b>2,345</b>
Ismani	2,466	2,455	2,350
Kilolo	2,465	2,454	2,349
Mufindi (Mafinga)	2,471	2,459	2,355
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,612</b>	<b>2,601</b>	<b>2,496</b>
Biharamulo	2,586	2,575	2,470
Karagwe (Kayanga)	2,628	2,617	2,512
Kyerwa (Ruberwa)	2,634	2,623	2,518
Muleba	2,612	2,601	2,496
Ngara	2,600	2,589	2,484
Misenyi	2,621	2,609	2,504
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,605</b>	<b>2,593</b>	<b>2,489</b>
Mlele (Inyonga)	2,586	2,575	2,470
Mpimbwe (Majimoto)	2,597	2,586	2,481
<b>Kigoma</b>	<b>2,628</b>	<b>2,617</b>	<b>2,512</b>
Uvinza (Lugufu)	2,640	2,629	2,524
Buhigwe	2,617	2,606	2,501
Kakonko	2,585	2,574	2,469
Kasulu	2,614	2,603	2,498
Kibondo	2,592	2,581	2,476
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>2,482</b>	<b>2,427</b>	<b>2,271</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,485	2,430	2,275
Mwanga	2,475	2,420	2,264
Rombo (Mkuu)	2,498	2,444	2,288
Same	2,468	2,413	2,258
Siha (Sanya Juu)	2,488	2,433	2,278
<b>Lindi</b>	<b>2,381</b>	<b>2,357</b>	<b>2,339</b>
Lindi-Mtama	2,386	2,362	2,357
Kilwa Masoko	2,405	2,381	2,314
Liwale	2,417	2,393	2,360
Nachingwea	2,401	2,377	2,369
Ruangwa	2,407	2,383	2,370
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,526</b>	<b>2,471</b>	<b>2,316</b>
Hanang (Katesh)	2,537	2,482	2,326
Kiteto (Kibaya)	2,541	2,487	2,331
Mbulu	2,539	2,484	2,329
Simanjiro (Orkasumet)	2,558	2,503	2,348

<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,575</b>	<b>2,564</b>	<b>2,459</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,616	2,605	2,500
Rorya (Ingirijuu)	2,584	2,573	2,468
Rorya (Shirati)	2,619	2,608	2,503
Bunda	2,566	2,555	2,450
Butiama	2,572	2,561	2,456
Serengeti (Mugumu)	2,621	2,610	2,505
Tarime	2,586	2,575	2,470
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,591	2,580	2,475
<b>Mbeya</b>	<b>2,504</b>	<b>2,492</b>	<b>2,388</b>
Chunya	2,513	2,502	2,397
Chunya (Makongolosi)	2,527	2,516	2,411
Kyela	2,519	2,508	2,403
Mbarali (Rujewa)	2,488	2,477	2,372
Rungwe (Tukuyu)	2,513	2,501	2,397
<b>Morogoro</b>	<b>2,422</b>	<b>2,410</b>	<b>2,305</b>
Mikumi	2,437	2,426	2,321
Kilombero (Ifakara)	2,459	2,448	2,343
Kilombero (Mlimba)	2,482	2,471	2,366
Kilombero (Mngeta)	2,471	2,460	2,355
Ulanga (Mahenge)	2,470	2,459	2,354
Malinyi	2,480	2,469	2,364
Kilosa	2,440	2,429	2,324
Gairo	2,440	2,429	2,324
Mvomero (Wami Sokoine)	2,432	2,421	2,316
Turiani	2,447	2,435	2,331
<b>Mtwara</b>	<b>2,368</b>	<b>2,344</b>	<b>2,353</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,404	2,380	2,402
Masasi	2,384	2,360	2,379
Newala	2,388	2,364	2,385
Tandahimba	2,382	2,358	2,378
Nanyamba	2,382	2,358	2,378
<b>Mwanza</b>	<b>2,547</b>	<b>2,535</b>	<b>2,431</b>
Kwimba	2,565	2,553	2,449
Magu	2,555	2,544	2,439
Misungwi	2,541	2,530	2,425
Sengerema	2,579	2,568	2,463
Ukerewe	2,606	2,595	2,490
<b>Njombe</b>	<b>2,489</b>	<b>2,478</b>	<b>2,373</b>
Njombe (Kidegembye)	2,510	2,498	2,394
Ludewa	2,527	2,516	2,411
Makambako	2,481	2,470	2,365
Makete	2,520	2,509	2,404
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,487	2,476	2,371
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,570</b>	<b>2,558</b>	<b>2,453</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,570	2,558	2,453
Kalambo (Matai)	2,577	2,566	2,461
Nkasi (Namanyele)	2,583	2,572	2,467

<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>2,453</b>	<b>2,429</b>	<b>2,404</b>
Mbinga	2,466	2,442	2,438
Namtumbo	2,444	2,420	2,433
Nyasa (Mbamba Bay)	2,491	2,467	2,440
Tunduru	2,418	2,394	2,463
<b>Shinyanga</b>	<b>2,525</b>	<b>2,514</b>	<b>2,409</b>
Kahama	2,539	2,528	2,423
Kishapu	2,554	2,543	2,438
Ushetu (Nyamilangano)	2,557	2,545	2,441
Simiyu (Bariadi)	2,567	2,556	2,451
Busega (Nyashimo)	2,560	2,549	2,444
Itilima (Lagangabilili)	2,570	2,559	2,454
Maswa	2,558	2,547	2,442
Meatu (Mwanhuzi)	2,565	2,554	2,449
<b>Singida</b>	<b>2,487</b>	<b>2,476</b>	<b>2,371</b>
Iramba	2,499	2,488	2,383
Manyoni	2,472	2,460	2,356
Ikungi	2,483	2,472	2,367
Mkalama (Nduguti)	2,512	2,501	2,396
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,513</b>	<b>2,502</b>	<b>2,397</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,520	2,509	2,404
Ileje	2,517	2,506	2,401
Momba (Chitete)	2,522	2,511	2,406
Tunduma	2,517	2,506	2,401
<b>Tabora</b>	<b>2,551</b>	<b>2,540</b>	<b>2,435</b>
Igunga	2,505	2,493	2,389
Kaliua	2,570	2,559	2,454
Ulyankulu	2,564	2,553	2,448
Nzega	2,515	2,504	2,399
Sikonge	2,563	2,551	2,447
Urambo	2,564	2,553	2,448
Uyui	2,552	2,541	2,436
<b>Tanga</b>	<b>2,435</b>	<b>2,381</b>	<b>2,225</b>
Handeni	2,456	2,401	2,246
Kilindi	2,471	2,416	2,261
Korogwe	2,448	2,393	2,237
Lushoto	2,457	2,402	2,247
Mkinga (Maramba)	2,442	2,388	2,232
Muheza	2,440	2,385	2,230
Pangani	2,442	2,387	2,232

## B: BEI ZA JUMLA

<b>Bei za Jumla - DSM</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,272.01</b>	<b>2,260.45</b>	<b>2,156.58</b>

<b>Bei za Jumla - TANGA</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,310.79</b>	<b>2,255.77</b>	<b>2,101.39</b>

<b>Bei za Jumla - MTWARA</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,243.18</b>	<b>2,218.87</b>	

**Nzinyangwa E. Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**